
USAID
KUTOKA KWA WATU
WA MAREKANI




*Deus Kibamba, aliyekuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA) akifanya mapitio ya marekebisho ya vipengele vya Sheria ya Vyama Vya Siasa na washiriki wa warsha*

*Picha na: NDI*

# TANZANIA

## *TUSHIRIKI PAMOJA*

Mradi wa Tushiriki Pamoja unalenga kuimarisha na kusaidia jamii, hasa wanawake, vijana, na watu wanaoishi na ulemavu, kushiriki, na kukuza michakato ya kisiasa ya uwajibikaji na iliyo jumuishi; uangalizi wa uchaguzi wenye ufanisi; mifumo ya kisiasa jumuishi na shindani; uwazi mkubwa katika uandaaji na usimamiaji wa chaguzi; na kufanya marejeo mara baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Mradi huu unakusudia kuboresha uwezo wa taasisi na mashirika husika kuwajibika katia kipindi chote cha mzunguko wa uchaguzi nchini Tanzania cha kupitia ushiriki wa wapiga kura, viongozi wenye ushawishi, na taasisi zinazoandaa na kusimamia chaguzi, , wakati huo huo ukijenga muungano wa vyama vya , vya kiraia vyenye milengo ya kidemokrasia, na kuongeza taratibu za ndani ya vyama vya siasa ili kukuza ushiriki wa wanawake, vijana, na watu wanaoishi naulemavu katika shughuli za demokrasia.

Mradi wa CEPPS unalenga sekta zote ili kushughulikia mahitaji maalum na vizuizi vya ushiriki vinavyowakabili watu wa makundi yanayodidimizwa nchini Tanzania, hasa wanawake, vijana, na watu wanaoishi na ulemavu. Kwa kuunga mkono majukwaa ya mazungumzo na elimu ya uraia na mpigakura, na kuendeleza mashirikiano kati ya mitandao na vyama vya kiraia, , na wadau wa serikali, mradi huu wa miaka mitano utajenga misingi imara itakayopelekea kuwa na demokrasia jumuishi, hasa kwa makundi yanayodidimizwa.

## MATOKEO

- Umoja wa AZAKi za Kitanzania umeongeza washirika wake na kujiimarisha kama wanaharakati wanaoaminika na wanaoongoza kwa mageuzi ya kisiasa na ya chaguzi, ujumuishaji, na ushirikishaji wa wanawake, vijana na watu wanaoishi na ulemavu.
- AZAKI wanachama walishiriki katika kufanya marejeo ya miswada mbalimbaki nyeti (zikiwemo Sheria ya Vyama vya Siasa, Sheria ya Mashirika yasiyokuwa ya Serikali, , Sheria ya Takwimu, Sheria ya Makampuni, nk) huko Bungeni. Washirika waliratibu ushiriki wao, walitumia umuhimuwa nafasi zao, na kutokana na weledi wao, maoni yao kadhaa yameingizwa katika sheria zitazochangia ujumuishwaji.
- Juhudi za kuimarisha ushirikiano wa ndani na wa baina ya vyama vya siasa pamoja na mkutano wa kilele wa viongozi wa vyama vya upinzani. Waliainisha vipaumbele vingi vya pamoja, na walikubaliana upya juhudi za kushirikiana katika uchaguzi ujao.
- Kumefanyika maboresho ya miundo ya ndani ya uongozi katika mabaraza ya wanawake na vijana ya chama tawala na vyama vya upinzani yaliyopelekea kuboresha miundo ya ndani ya kiutawala na kuongeza uwiano wa makundi yote mawili ya wagombea na watoa maamuzi wa ndani ya chama. Mfano ACT Wazalendo walichagua mwanamke na mwanaume kijana kushika nafasi za makamu mwenyekiti na katibu wa chama.
- Washirika wa CEPPS waliainisha vinara na kujenga uhusiano miongoni mwa taasisi za kidemokrasia ndani ya Serikali ya Tanzania. Hii inajumuisha, Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, Msajili wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali, na Bunge. Matokeo yake, washirika walishiriki kutoa maoni na mapendekezo juu ya kanuni za uchaguzi wa serikali za mitaa, na walitoa michango ya mawazo yenye malengo ya kuendeleza ushirikishwaji na ushiriki wa makundi yanayodidimizwa kwenye muala ya , utawala wa demokrasia.
- Kuwezesha makundi ya waangalizi wa ndani wa uchaguzi kuangalia zoezi la uandikishaji wa piga kura kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.
- Mradi umewezesha taasisi mbili za kiraia kutoa elimu ya mpiga kura wakati wa uandikishaji wapiga kura na wakati wa uchaguzi. Watanzania 970035 walifikiwa na mradi.
- Mradi umewezesha vyama viwili vya siasa kupitia upya na kuborehsa ilani zao za uchaguzi kwa ajili ya uchaguzi wa mwaka 2020
- Kazi ya utetezi inayoungwa mkono kupitia Muungano wa Ushiriki unaozingatia ujumuishi wa vijana, watu wanaoishi na ulemavu na wanawake Tanzania Bara na Zanzibar.

**BAJETI:** Dola za Marekani 11,100,000

**MUDA**
Novemba 2017 – Novemba 2022

**MAENEO YA MRADI**
Nchi nzima

**MTEKELEZAJI**
Consortium of Elections and Political Process Strengthening:

- International Republican Institute (IRI)
- National Democratic Institute (NDI)
- International Foundation for Electoral Systems (IFES)

### MAWASILIANO YA USAID

Florida Henjewele
Afisa Mwakilishi wa Mkataba
+255 22 229 4490
fhenjewele@usaid.gov

**MAWASILIANO YA MTEKELEZAJI**

Peter Aling'o Okoth
Mkurugenzi wa Mradi

palingo@IRI.org

**KWA MAWASILIANO ZAIDI**

Tovuti: www.usaid.gov/tanzania
Facebook: USAIDTanzania
Twitter: @USAIDTanzania